



STRATEGIC  
IMPACT  
ADVISORS

Biashara Yake, Maisha Yake



# Usimamizi wa Kifedha

—  
Usimamizi wa Biashara na Ujuzi  
wa Kusoma na Kuandika wa  
Kidijitali kwa Wanawake  
Wajasiriamali Wadogo

*Ripoti hii imeweza kufanikishwa kwa ushirikiano wa ukarimu na watu wa Marekani kupitia Uwakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID). Muongozo huu ulitolewa chini ya Mradi wa Frontia za Kidijitali za DAI (Cooperative Agreement AID-OAA-A-17-00033) kutokana na ombi la USAID wakishirikiana na Mastercard.*

# Taaswira ya Moduli



## Jedwali la yaliyomo

**Sehemu ya 1:** Kutengeneza mpango wa kifedha na kutumia udhibiti wa kifedha 4

**Sehemu ya 2:** Kubainisha wajibu wako kwenye usimamizi wa kifedha 9

**Sehemu ya 3:** Kuelewa gharama za biashara yako 13

**Sehemu ya 4:** Kuelewa kwanini na vipi kuhusu uwekaji hesabu 17



## Malengo

1. Kujifunza jinsi ya kutengeneza mpango wa kifedha.
2. Kutambua aina ya rekodi na vitabu unavyofaa kutumia kwenye biashara yako.
3. Kuelewa jinsi simu yako inaweza kukusaidia uwekaji hesabu.

## Kwenye Moduli hii, unaweza...

- kuakisi wajibu wako kwenye usimamizi wa kifedha
- kujua gharama za biashara yako
- kufanya mazoezi ya uwekaji rekodi na uwekaji hesabu

# SEHEMU YA 1: KUTENGENEZA MPANGO WA KIFEDHA NA KUTUMIA UDHIBITI WA KIFEDHA

## Malengo:

1. Kuelewa kwanini unahitaji mpango wa kifedha.
2. Kuelewa faida za kufuata mpango wa kifedha na kutumia udhibiti wa kifedha.



# Biashara Yako Inahitaji Mpango wa Kifedha

**Ikiwa huna mpango wa kifedha ambao umeweka, ni vigumu sana kudhibiti kuhusu jinsi unavyotumia pesa zako.**

Wakati unatengeneza mpango, angalia ndoto zako za muda mfupi na muda mrefu.

Udhibiti wa kifedha utakusaidia kusimamia fedha za biashara yako.

**Udhibiti wa kifedha ni nini?**

**Kwanini udhibiti wa kifedha ni muhimu kuendesha biashara?**



# Udhibiti wa Kifedha


**Udhibiti wa kifedha maana yake ni kuelewa fedha za duka lako.**

Inahusisha kuchukua hatua za kutengeneza pesa zaidi kwenye mauzo kuliko gharama zako, usimamizi wa gharama zako, na kuweka akiba ya pesa kwa gharama zisizotarajiwa.

Ukiwa na ruwaza ya utumiaji unaodhibitiwa na mpango wa bajeti ya kila mwezi, unaweza kutumia mikakati kufikia malengo yako ya kibiashara na ukuaji.



# Mpango Mzuri wa Kifedha na Udhhibiti wa Kifedha Unasaidia Kwa...



**Kufuatilia na usimamizi wa gharama**



**Kufuatilia orodha ya mali**



**Kudumisha uchanya wa mapato halisi (kuingia na kutoka kwa pesa taslimu)**



**Ulipaji wa bili kwa wakati**



**Kupokea malipo haraka kwa wateja**



**Kuboresha utendaji bora na ujuzi wa mashauriano**

## **Wajibika kwa Matumizi Yako**


Kufuatilia matumizi yako kunakufanya kuwajibika kusimamia pesa zako. Ikiwa unajua kuwa utakuwa unakagua matumizi yako kila wiki, unaweza kujipatia motisha kufikiria mara mbili kabla ya kununua kitu ambacho hakipo kwenye mpango wako. Wakati unatengeneza udhibiti wako wa kifedha, utaona jinsi kufuata mpango kunasaidia kufikia malengo yako.

## **Mafanikio ya Udhibiti wa Kifedha**

Inaweza isionekane kupunguza ununuzi mara moja, lakini kuwa na udhibiti wa kifedha unaleta mafanikio baada ya muda mrefu. Kuishi kulingana na hali yako kunaweza kukupunguzia kiwango cha msongo wa mawazo na kuhakikisha kuwa una pesa za kununua vitu ambavyo kweli unavihitaji.

## SEHEMU YA 2: KUBAINISHA WAJIBU WAKO KWENYE USIMAMIZI WA KIFEDHA

**Malengo:** Kugundua jinsi wanawake na wanaume wanaweza kushirikiana kutoa maamuzi kwa biashara.



Wanaume na wanawake wote wanaweza kuwa na wajibu kwenye kusimamia fedha za biashara!



???

Nani  
anasimamia  
fedha za  
biashara yako?

Ni jinsi gani  
unaweza kufuatilia  
pesa taslimu  
zinazoingia na  
kutoka kwenye  
biashara yako?



# Wajibu Wako ni Upi Kwenye Kusimamia Pesa Kwenye Biashara?

**Je, unasimamia mambo yoyote ya kifedha ya biashara yako au nyumbani?**

**Je, wajibu wako kama mwanamke unaushawishi wajibu wako kwenye biashara?**

1. Kama mwanamke, je, unakutana na vikwazo vyovyote kwenye kupata maelezo au kuelewa maelezo yanayohusiana na fedha nyumbani au kwenye biashara yako?
2. Je, kuna migawanyiko ya kijinsia kwenye kufanya maamuzi ya kifedha ya biashara? Ikiwa ndio, kwanini kuna migawanyiko hii?
3. Unakubaliana na migawanyiko hiyo, au ungependa kuibadilisha?
4. Familia na biashara zina faidi vipi wakati mwanamke anashiriki kufanya maamuzi?

## Wakati wanawake wanasaidia kusimamia fedha, kuna nafasi ya kuongezeka kukua kwa biashara na kunawiri.

Ushirikiano wa wanawake kwenye fedha za dukani na uendeshaji utaleta ujuzi tofauti kwenye biashara.

Ushirikiano wa wanawake kwenye biashara pia unaongeza nguvu kazi na maarifa kwenye biashara.

Ukifanya kazi dukani, unaweza kuamua jinsi pesa zinatumiwa – na kuzingatia kujilipa mshahara wa mwezi au kuweka pesa za familia pembeni.

**Mabadiliko  
yanawezekana!**



## SEHEMU YA 3: KUELEWA GHARAMA ZA BIASHARA YAKO

**Malengo:** Kutambua aina ya gharama tofauti na viwango kwenye biashara yako.



Sasa  
tutambue  
gharama  
za biashara  
yako!

# Kwanini Unahitaji Pesa Kwa Biashara Yako?



# Kufuatilia Gharama za Biashara Yako

## Gharama za Biashara Yangu

Kodi ya nyumba

Malipo ya mkopo

Vifaa/Bidhaa

Umeme

Matengenezo ya mjengo au kifaa

Usafiri na Mizigo

Mishahara

Kodi

Simu

Bima





Ili uweze kumudu hizi gharama, njia zako za kupata mapato ni zipi? Na unapanga vipi hizi gharama?




Ni changamoto gani unapitia unapomudu hizi gharama?

## SEHEMU YA 4: KUELEWA KWANINI NA VIPI KUHUSU UWEKAJI HESABU

### Malengo:

1. Kuelewa jinsi ya kuweka vitabu rasmi ili kufuatilia fedha za biashara yako.
2. Kujifunza vidokezo vya kutumia simu yako kwa uwekaji hesabu.
3. Kuwa na ujuzi wako wa uwekaji hesabu kwa kufanya mazoezi.



Uko tayari  
kufanya  
mazoezi ya  
uwekaji  
hesabu?



# Uwekaji Rasmi Rekodi za Biashara Yako: Umuhimu wa Uwekaji Hesabu



**1** Kujua mapato ya duka lako na gharama wakati wowote ule.



**2** Kuhesabu gharama zako za kila mwezi kama vile kodi ya nyumba, umeme, gharama za simu, na mishahara.



**3** Kuelewa ikiwa duka lako linapata faida au la.



**Sasa  
Tujadili!**



**Unafuatilia vipi fedha za biashara zako?**


- A. Nazifuatilia akilini au kwa kuweka risiti.
- B. Naandika mauzo na gharama kwa kijitabu cha maelezo.
- C. Natumia simu yangu au kompyuta kurekodi mauzo na gharama.

**Ni mara ngapi unakagua ni kiasi gani umeuza na gharama zako?**

- A. Kila Siku
- B. Kila Wiki
- C. Kila Mwezi
- D. Mimi huangalia pesa kwenye till yangu au akaunti ya merchant mara kwa mara.

**Mtu Yeyote Anaweza  
Kufanya Uwekaji wa  
Hesabu Rahisi: Huhitaji  
Kuwa Mhasibu!**

**Unaweza kuweka hesabu kwa  
kutumia karatasi au programu:**



# Aina ya Vitabu



**KITABU CHA  
KUMBUKUMBU ZA  
BIASHARA YA KILA SIKU:**  
Kupata mauzo yako ya  
mwisho wa siku na ununuzi.



**SAJILI YA MIKOPO:**  
Kufuatilia madeni  
unayodai na  
kudaiwa.





**TAARIFA YA FAIDA NA  
HASARA:**  
Kufanya hesabu ikiwa  
biashara yako inapata  
faida au inapoteza  
pesa.

# Kutumia Simu Yako Ya Kisasa Kwa Uwekaji Hesabu


Kampuni zimetengeneza program za maduka madogo ambazo zinaweza kupatikana kukusaidia kufuatilia mauzo yako na gharama. Unahitaji simu ya kisasa kupakua hizi programu. Program zingine zinafikiwa kwenye kompyuta au tableti.

Kwa kuipakua programu kwenye simu yako ya kisasa, unaweza kuweka mauzo ya wateja na gharama, na kutengeneza rekodi moja kwa moja kwa simu yako. Hii inakusaidia kuona uhalisia wa jinsi ambavyo biashara yako inaendelea.






Weka shughuli kila wakati unapofanya mauzo au gharama.



Usisahau wale unaowadai pesa na kuwatumia ukumbusho wa malipo.



Angalia dashbodi ya programu yako uone utendaji wa duka lako na salio la pesa taslimu!

# Faida Ya Kutumia Udijitali Kwa Uwekaji Hesabu Wako

1

Ikiwa utatumia simu yako kwa uwekaji hesabu, utaweza kufikia rekodi zako kwa kuingia tu kwenye program kutoka kwa kifaa chochote. Huwezi kupoteza rekodi zako kama vile huwezi kupoteza kijitabu cha maelezo.

2


Kufuatilia shughuli za biashara yako mara kwa mara kwenye simu yako, kunasaidia kutengeneza rekodi za biashara yako. Unaweza kutumia hizi kuthibitisha kufuatilia rekodi za biashara yako ili kukusaidia kustahili kupata mkopo kwa wasambazaji au wakopeshaji.

3

Kampuni zinazotoa program za uwekaji hesabu zinaweza kukuunganisha na vyanzo vya mkopo au kukupatia “alama ya mkopo.”

4

Wengine kwenye biashara yako wanaweza kufikia programu kuweka rekodi na kutathmini shughuli ikiwa utawapa ruhusa ya kutumia programu.



**Unaweza kufikiria faida zingine zozote zaidi za kutumia program kwa uwekaji hesabu?**

**NYENZO YA KUFUNDISHIA**

Usimamizi wa Fedha Zako na Hey Sister




Masomo ya Hey Sister

Somo la 23: Nitasimamia vipi fedha za biashara yangu?





# Kuweka Rekodi za Mauzo na Gharama Kwenye Kitabu Chako Cha Kumbukumbu za Biashara ya Kila Siku



**Kuweka rekodi ya kila shughuli kwenye kitabu au kidijitali kutakusaidia kuweka kumbukumbu ya jinsi biashara yako inavyoendelea kwako wewe na wengine, kama benki na wasambazaji.**



# Faida za Kudumisha Vitabu vya Kumbukumbu vya Biashara Kila Siku


- ✓ Kudumisha maelezo kuhusu mauzo ya kila siku na ununuzi mahali pamoja.
- ✓ Kufuatilia pesa zako taslimu.
- ✓ Kuthibitisha mauzo na kuhesabu bidhaa zilizouzwa.
- ✓ Fuatilia pesa zilizotolewa dukani za mshahara wako.



# Nini Cha kujumuisha Kwenye Kitabu cha Kumbukumbu za Biashara ya Kila Siku

Tarehe	Mauzo				Ununuzi			Gharama mbalimbali zinazoweza kutokea
	Pesa taslimu	Pesa zilizopo benki (ATM / Kidijitali)	Mkopo		Ununuzi wa pesa taslimu	Mkopo		
			Mauzo ya mkopo	Kupokea pesa taslimu		Kununua kwa mkopo	Malipo ya pesa taslimu	
01/01/2022	1,500	500	200				200-usafiri	
02/01/2022	1,300		400	200	1,500	400	400-bili ya umeme	
<b>Jumla ya Kila Mwezi</b>								





# Kipindi cha Kufanya Mazoezi

---




- Tarehe 01/03/2021, Sofía na Mateo waliuza bidhaa za jumla ya 3,000. Wateja wao walilipa kwa njia tofauti. Wateja walilipa pesa taslimu 2,000, 500 kwa malipo ya kidijitali (k.v mobile money), na mteja mmoja akanunua bidhaa zenye thamani ya 500 kwa mkopo.
- Tarehe 02/03/2021, Mteja mmoja wa Sofía na Mateo alilipa mkopo wake wa 300. Sofía na Mateo pia walimuuzia mteja bidhaa za 2,500 na akalipa pesa taslimu. Sofía na Mateo walikubaliana kutumia 300 za mapato yao ya duka kununulia bidhaa zaidi.
- Tarehe 03/03/2021, Mteja wa kawaida alinunua bidhaa za 1,000, alafu Sofía na Mateo wakakubaliana anunue kwa mkopo. Sofía pia alizungumza na msambazaji na akanunua bidhaa kwa mkopo zenye thamani ya 500.
- Tarehe 03/03/2021, Mateo alilipa kodi ya duka ya kila mwezi ya 5,000 na Sofía akatumia akaunti ya pochi ya simu kulipa bili ya umeme ya 400.
- Tarehe 04/03/2021, Mateo na Sofía walitumia 500 kulipa deni la msambazaji ambaye aliwauzia bidhaa kwa mkopo mwezi uliotangulia.

**Jaza Kitabu cha kumbukumbu za biashara ya kila siku kulingana na haya maelezo.**



Tarehe	Mauzo				Ununuzi			Gharama mbalimbali zinazoweza kutokea
	Pesa taslimu	Pesa zilizopo benki (ATM / Kidijitali)	Mkopo		Ununuzi wa pesa taslimu	Mkopo		
			Mauzo ya mkopo	Kupokea pesa taslimu		Kununua kwa mkopo	Malipo ya pesa taslimu	
01/03/2021	2,000	500	500					
02/03/2021	2,500			300			300-bidhaa	
03/03/2021			1,000			500		
04/03/2021							500	
<b>Jumla ya Kila Mwezi</b>	<b>4,500</b>	<b>500</b>	<b>1,500</b>	<b>300</b>		<b>500</b>	<b>500</b>	
							<b>5,700</b>	



# Sajili za Mkopo



Kuna aina mbili za sajili za mkopo: Sajili za mkopo wa mteja na sajili za mkopo wa msambazaji.




# Aina za Sajili za Mkopo

Mkopo wa mteja (Akaunti ya kulipa)						
Jina la mteja	Tarehe	Jina la msambazaji	Maelezo	Thamani kitu kilichouzwa/kununuliwa kwa mkopo	Kiwango kilicholipwa	Salio
Max	03/04/2021	AB Wholesaler	Mgawo: Mchele, Sukari (Kilo moja moja)	500	300	200
Emma	19/04/2021	AB Wholesaler	Sabuni, Shampoo, Biskuti, Chumvi, Mafuta ya kupikia	300	150	150



Mkopo wa wasambazaji (Akaunti ya kulipwa)					
Tarehe	Jina la Msambazaji	Maelezo	Thamani ya kitu kilichouzwa/kilichonunuliwa kwa mkopo	Kiwango kilicholipwa	Salio
03/03/2021	AB Wholesaler	Mchele, Unga	500		500
04/03/2021	AB Wholesaler	Mchele, Unga		500	0





# Kipindi cha Kufanya Mazoezi

---



# Tukio la 1


- Tarehe 05/03/2021, Grace alinunua vitu vifuatavyo dukani kwako:
  - kilo 1 ya mchele kwa 40
  - kilo 1 ya maharagwe kwa 80
  - kilo 1 ya sukari kwa 70
- Tarehe 07/03/2021, Grace alinunua,
  - kilo 5 za ngano kwa 100
  - siku hiyo hiyo, akalipa pia 200 pesa taslimu.

**Jaza sajili ya mkopo ya tarehe 07/03/2021 kulingana na haya maelezo.**



## Sajili ya Mkopo ya Wateja (Akaunti ya kulipa)

Tarehe	Mteja	Maelezo	Thamani ya kitu kilichouzwa / kilichonunuliwa kwa mkopo	Kiwango kilicholipwa	Salio
Grace	05/03/2021	Mgawo: Maharagwe, Mchele, Sukari (Kilo moja moja)	190		190
Grace	7/03/2021	Kilo 5 za Ngano	100	200	90



## Tukio la 2

- Tarehe 07/04/2022, ulinunua bidhaa kutoka kwa AB Wholesaler kwa mkopo.
  - mchele kilo 20 kwa 1,000
  - mikebe kumi ya gramu 100 ya Nescafe Classic Coffee kwa 1,000
- Tarehe 11/04/2022, ulinunua bidhaa zaidi kwa mkopo.
  - miche 40 ya Dove Soap kwa 1,200
  - chupa kumi za mililita 100 za Pantene Shampoo kwa 2,000
- Tarehe 15/04/2022, ulilipa 600 kwa AB Wholesaler kupunguza mkopo wako.

**Jaza sajili ya mkopo kulingana na haya maelezo.**



## Sajili ya Mkopo ya Msambazaji (Akaunti ya Kulipwa)

Tarehe	Msambazaji	Maelezo	Thamani ya kitu kilichouzwa / kilichonunuliwa kwa mkopo	Malipo	Salio
07/04/2022	AB Wholesaler	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kilo 20 za mchele kwa 1,000</li> <li>Chupa kumi za gramu 100 za Nescafe Classic Coffee kwa 1,000</li> </ul>	2,000		2,000
11/04/2022	AB Wholesaler	<ul style="list-style-type: none"> <li>Miche 40 ya Dove Soap kwa 1,200</li> <li>Chupa kumi za mililita 100 za Pantene Shampoo 2,000</li> </ul>	3,200		3,200
15/04/2022	AB Wholesaler			600	4,600





**Tumia udhibiti wa  
kifedha kusimamia  
mkopo wa  
msambazaji.**

Wakati unanunua bidhaa kutoka kwa wauzaji wa jumla kwa mkopo, walipe kwa wakati ili kuhakikisha kuwa bidhaa zako unaletewa.


- Nini kitakachotokea ikiwa hutalipa wauzaji wa jumla kwa wakati?
- Utafanya nini ikiwa hutalipa wauzaji wa jumla kwa wakati?

**Sasa  
tujadili!**



Unafikiria kwamba  
kujaza kitabu cha  
kumbukumbu za  
biashara ya kila siku  
na sajili za mkopo  
itakusaidia na  
biashara yako?

Ni faida na hasara  
gani unazoziona  
kwenye kudumisha  
hivi vitabu?



# Taarifa ya Faida na Hasara ya Kila Mwezi



- Taarifa ya Faida na Hasara ni taarifa ya kifedha ambayo inatoa maelezo mafupi ya mapato ya biashara, gharama na matumizi yaliyopatikana baada ya muda fulani.
- Taarifa ya Faida na Hasara inaonyesha uwezo wa biashara na kutoweza kupata mauzo na kusimamia gharama.





## Taarifa ya Faida na Hasara ya Kila Mwezi

<b>Maelezo</b>	<b>Yakuandikwa kwa Faida na Hasara</b>
Mauzo ya pesa taslimu	(Malipo ya pesa taslimu na kidijitali)
Mauzo ya mkopo	
<b>Jumla ya Mapato</b>	<b>Mauzo ya Pesa Taslimu + Mauzo ya Mkopo</b>
Jumla ya gharama ya vitu/vilivyouzwa	= Kifungua biashara + ununuzi wa pesa taslimu + ununuzi wa mkopo – kifunga biashara
Jumla ya gharama ya usafirishaji	
Jumla ya kiwango kilicholipwa kodi ya duka	
Jumla ya kiwango kilicholipwa umeme	
Jumla ya kiwango kilicholipwa wafanyikazi	
Jumla ya kiwango kilichotolewa na mwenye(we) duka kwa matumizi binafsi	
Jumla ya gharama za simu	
Gharama zingine zilizopatikana	
<b>Jumla ya Gharama</b>	
<b>Faida halisi – kufanyiwa hesabu</b>	<b>Jumla ya Mapato – Jumla ya Gharama</b>



- **Gharama ya bidhaa zilizouzwa:**

Gharama ya bidhaa zilizouzwa = kifungua biashara + ununuzi wa pesa taslimu – ununuzi wa mkopo – kifunga biashara

- **Jinsi ya kupata kifunga biashara?**

Sajili ya bidhaa lazima iwepo dukani pale ambapo ununuzi wa vitu na mauzo vinarekodiwa. Kutoka hapo, thamani ya kifunga biashara inaweza kuhesabiwa. Ikiwa sajili ya bidhaa haikudumishwa, basi kuhesabu kwa macho kwa orodha ya mali lazima kufanyike.

**Faida Halisi = Mapato - Gharama**






# Tengeneza Taarifa ya Faida na Hasara ya Duka la Sofía na Mateo

---





# Kitabu cha Kumbukumbu za Biashara ya Kila Siku cha Duka la Sofía na Mateo


---



Tarehe	Mauzo				Ununuzi			Gharama mbalimbali zinazoweza kutokea
	Pesa taslimu	Pesa zilizopo benki (ATM / Kidijitali)	Mkopo		Ununuzi wa pesa taslimu	Mkopo		
			Mauzo ya mkopo	Kupokea pesa taslimu		Kununua kwa mkopo	Malipo ya pesa taslimu	
01/01/2021	645		110					
02/01/2021	486		45				200-usafiri	
03/01/2021	768	500	65	60	1,250			
04/01/2021								
05/01/2021	984		132	80			400-umeme	
06/01/2021	648		230	50	2,500			
07/01/2021	864		117					
08/01/2021	1,045	200	28	120			800-kutoa pesa kwa matumizi binafsi	
09/01/2021	987		45	100				
10/01/2021	459		458	220			200-simu	
11/01/2021	855		128	60				



Tarehe	Mauzo				Ununuzi			Gharama mbalimbali zinazoweza kutokea
	Pesa taslimu	Pesa zilizopo benki (ATM / Kidijitali)	Mkopo		Ununuzi wa pesa taslimu	Mkopo		
			Mauzo ya mkopo	Kupokea pesa taslimu		Kununua kwa mkopo	Malipo ya pesa taslimu	
12/01/2021	1,290		35	123	2,580	700		
13/01/2021	980		235	80				
14/01/2021	1,239		335	115				
15/01/2021	1,453		25	85	1,480			
16/01/2021	1,267		231	45				
17/01/2021								
18/01/2021	910	300	443	278	650			
19/01/2021	1,576		34	135	3,275		400	
20/01/2021	1,086		543	328				
21/01/2021	987	1,000	245					
22/01/2021	110		453	225	875			



Tarehe	Mauzo				Ununuzi			Gharama mbalimbali zinazoweza kutokea
	Pesa taslimu	Pesa zilizopo benki (ATM / Kidijitali)	Mkopo		Ununuzi wa pesa taslimu	Mkopo		
			Mauzo ya mkopo	Kupokea pesa taslimu		Kununua kwa mkopo	Malipo ya pesa taslimu	
23/01/2021	1,286		354	55				
24/01/2021								
25/01/2021	786		435	288	2,470	800	200	
26/01/2021	1,453		334	145				
27/01/2021	1,208		234	254				
28/01/2021	897		434	650	5,200	900	750	2,000-ununuzi wa mali
29/01/2021	1,234		45	35				
30/01/2021	876		320	425	4,580		500	1,000-mishahar
31/01/2021	987		136	125				2,000-kodi ya duka
<b>JUMLA</b>	<b>27,366</b>	<b>2,000</b>	<b>6,229</b>	<b>4,081</b>	<b>24,860</b>	<b>2,400</b>	<b>1,850</b>	<b>6,600</b>



## Taarifa ya Faida na Hasara ya Kila Mwezi

Maelezo	Yakuandikwa kwa Faida na Hasara
Mauzo ya pesa taslimu	29,366
Mauzo ya mkopo	6,229
<b>Jumla ya Mapato</b>	<b>35,595</b>
Jumla ya gharama ya vitu/vilivyouzwa	27,260
Jumla ya gharama ya usafirishaji	200
Jumla ya kiwango kilicholipwa kodi ya duka	2,000
Jumla ya kiwango kilicholipwa umeme	400
Jumla ya kiwango kilicholipwa wafanyikazi	1,000
Jumla ya gharama za simu	200
Jumla ya kiwango kilichotolewa na mwenye(we) duka kwa matumizi binafsi	800
Gharama zingine zilizopatikana (ununuzi wa mali)	2,000
<b>Jumla ya Gharama</b>	<b>33,860</b>
<b>Faida halisi (35,595 – 33,860 = 1,735)</b>	<b>1,735</b>






# Sasa Elezea!



Hadi kufikia  
sasa,  
umejifunza:



# Mambo ya Kukumbuka

1




**Kuweka fedha zako binafsi na za biashara tofauti.**

2




**Kujua gharama zako na vyanzo vya mapato yako.**

3



**Fanya mazoezi rahisi ya uwekaji hesabu:**

- Weka rekodi za shughuli zako za kibiashara.
- Kupanga na kufanya bajeti ya biashara yako.
- Imarisha kukuza biashara yako.



**Leo  
umejifunza  
nini?**




**Ni kipi ulichoona  
kinafaa ambacho  
utakitumia  
kusimamia fedha  
zako?**



**Utatumia mbinu za  
uwekaji hesabu  
ulizogundua  
kwenye biashara  
yako?**





**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI

STRATEGIC  
**IMPACT**  
ADVISORS



[www.siaedge.com](http://www.siaedge.com)

Laini ya Pili  
Laini ya Tatu

